



**THE TANZANIA ECONOMY: RECOVERY FROM COVID-19 PANDEMIC AND  
BEYOND**

PROCEEDINGS OF THE 20<sup>TH</sup> CONFERENCE OF FINANCIAL INSTITUTIONS HELD AT JAKAYA  
KIKWETE CONVENTION CENTRE, DODOMA

25<sup>TH</sup> AND 26<sup>TH</sup> NOVEMBER 2021

© **Bank of Tanzania 2021**

For any inquiry please contact:

Director of Economic Research and Policy

Bank of Tanzania, 16 Jakaya Kikwete Road 40184, P.O. Box 2302, Dodoma,

Telephone: +255 22 223 3328

Email: [botcommunications@bot.go.tz](mailto:botcommunications@bot.go.tz)

## Foreword



Since the last Conference of Financial Institutions (19<sup>th</sup> COFI) held in 2019, the country has sailed through a number of turbulences, some of which are highlighted in Bank of Tanzania's routine economic publications. Standing high in that list are the outbreak of the COVID-19 pandemic with the associated challenges on economies; and the decline in growth of banks credit to private sector, partly contributed by slowdown in demand and banks' cautious stance in lending and further exacerbated by the pandemic. These reinvigorated the debate on and the need for leveraging technology in business management, marketing, and service delivery. Parallel to that is the push for use of private digital currencies (crypto currencies) in which countries have reacted differently, owing to risks associated with them. In response, central banks across the globe are thinking of and weighing their options with regards introducing central bank digital currencies as an alternative.

Against this background, the Bank organised the 20<sup>th</sup> COFI under the theme "The Tanzania Economy: Recovery from Covid-19 Pandemic and Beyond" to stimulate debate on some of these issues, largely benefiting from, among others, renowned and experienced practitioners, researchers, business persons, and members of the civil society.

This booklet provides proceedings of the deliberations, largely highlighting on:

- Priorities and policy options that can facilitate increased utilisation of resources and growth in productivity for fast recovery of the economy;
- Ways to exploit advantages offered by digital technologies in accelerating economic growth and recovery in the aftermath of COVID-19 pandemic;
- Experiences on central bank digital currencies and crypto currencies; and
- Measures that can help increase growth of banks credit to private sector and lowering cost of funds.

The Bank is heartily grateful to all participants for their insightful contributions, which have made this booklet a reality. My sincere hope is that you will find this booklet useful.

Prof. Florens D. A. M. Luoga

**GOVERNOR**



## Acknowledgement

We are grateful to Bank of Tanzania Executive Office, Prof. Florens D.A.M Luoga (Governor), and Deputy Governors: Dr. Yamungu Kayandabila, Mr. Julian Banzi, and Dr. Bernard Kibesse; and Tanzania Bankers Association (TBA) chairperson, Mr. Abdulmajid Nsekela for their guidance in the preparation of the 20<sup>th</sup> COFI.

Our gratitude also goes to the technical bench, including Dr. Suleiman Missango, Mr. Kened Nyoni, Dr. Wilfred Mbowe, Dr. Nicholas Kessy, Dr. Lorah Madete, Mr. Dominic Mwita, Mr. Rweyemamu Barongo, Mr. Lwaga Mwambande, Ms. Tusekelege Joune and Ms. Happiness Naumanga who devoted their precious time to write this booklet. Our thanks also go to the rapporteurs of the conference, including Ms. Nangi Massawe, Dr. Majige Budeba, Ms. Gloria Mbiha, Mr. John Mero, Dr. Anna Lyimo, Ms. Khadijah Kishimba and Dr. Eng. Sigsbert Rwiza. Last but not least are the resource persons and participants for accepting to set aside their time and sharing their vast experiences and knowledge on the conference topics leading to the manuscript of this booklet.

## Contents

<b>Foreword</b> .....	<b>iii</b>
<b>Acknowledgement</b> .....	<b>v</b>
<b>PART I: OPENING CEREMONY</b> .....	<b>7</b>
1.1 Sala.....	1
1.2 Salamu za Mkoa Kutoka kwa Mh. Anthony Mtaka, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma.....	2
1.3 Salamu Kutoka kwa Bw. Abdulmajid Nsekela, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Mabenki Tanzania..	3
1.4 Maneno ya Utangulizi Kutoka kwa Prof. Florens D.A.M. Luoga, Gavana Benki Kuu ya Tanzania .....	4
1.5 Salamu za Ukaribisho kutoka kwa Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba, Waziri wa Fedha na Mipango .....	12
1.6 Hotuba ya Ufunguzi ya Mgeni Rasmi, Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania .....	16
<b>PART II: SUMMARY OF PRESENTATIONS AND DISCUSSIONS</b> .....	<b>21</b>
2.1 Session One: Economic Growth and Sustainability During and Beyond COVID-19 Pandemic: Priorities and Policy Options.....	22
2.2 Session Two: Accelerating Digitalization for Recovery and Sustainable Growth .....	26
2.3 Session Three: Digital Currencies: Experiences, Risks, and Regulatory Issues.....	31
2.4 Session Four: Scaling up Private Sector Credit Beyond COVID-19 Pandemic: Role of Government, Financial Institutions and Private Sector .....	36
<b>PART III: CLOSING</b> .....	<b>39</b>
3.1 Remarks by Dr. Yamungu Kayandabila, Deputy Governor Bank of Tanzania .....	40

## **PART I: OPENING CEREMONY**

## 1.1 Sala

### **Jumuiya ya Kikristo Tanzania (Askofu Joseph Mtolela)**

Mwenyezi Mungu Baba wa milele na Baba wa Bwana Yesu Kristo, tunakushukuru kwa rehema na upendo wako mkuu. Uko pamoja nasi katika kusanyiko hili. Tunakushukuru sana kwa ajili ya Mhe. Rais wetu Samia Suluhu Hassan, uliyemteua kuongoza nchi hii kwa awamu ya sita. Tunakushukuru vilevile Mungu wetu, ulivyotupitisha katika janga hili la UVIKO-19. Janga ambalo Mungu limeitikisa dunia, lakini Tanzania imesimama katika umoja, upendo na mshikamano. Kwa neema yako Mungu, kupitia hekima za Mhe. Rais, tumepata chanjo ambayo Mungu bado tunakuomba uzidi kuwagusa wengine ambao hawajaelewa maana yake, wapate kuguswa na kupata neema hii.

Tunakushukuru pia kwa taasisi zetu za fedha Mungu wetu, hasa Benki Kuu ambayo inasimamia taasisi zote` za fedha nchini, kuendelea kuibariki na kuiongoza Mungu wetu mtakatifu. Ni taasisi ambayo ni kiini cha uchumi wetu, neema yako iibariki taasisi hii. Wabariki wote wanaosimamia, hata Mhe. Gavana. Neema yako iwafunike wote, hata Mhe. Waziri wa Fedha na wote Mungu wetu.

Kwa Mhe. Rais, endelea kumgusa, endelea kumwongoza na mapenzi yako mema na matukufu Mungu wetu mtakatifu, nchi ikae katika hali njema. Hata sisi tunaoendelea kutumika kwa namna yoyote ile, katika dini, katika sekta binafsi katika siasa, neema yako itufunike. Ni katika jina la Baba, na Mwana na Roho Mtakatifu, tunaomba tukikuamini. Amina.

### **Baraza la Maaskofu Tanzania (Padre Jubbie Augustine)**

Kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu. Amina.

Mungu Baba Mwenyezi tunakushukuru sana kwa siku hii ya leo, tunapona kwamba neema na baraka umetujalia sisi sote, hasa kuanzia viongozi, kwa nchi yenyewe na viongozi wote waliopo hapa na uliowachagua wote wafike hapa. Tunakushukuru sana kwa afya zetu, tunakushukuru sana kwa mipango yote uliyotupangia katika maisha yetu, na katika nchi yetu.

Mungu Baba, wewe mwenyewe ulitamka kupitia Injili ya Luka 14:28, unapoanza kupanga chochote, ukae kwanza chini halafu uanze kufikiria na kupanga vizuri. Sasa leo tunapopanga juu ya hayo mambo na maendeleo ya nchi yetu, uwe pamoja nasi na utuongoze ili tunapoanza kuvuka na yale majanga na matatizo mbalimbali, tujue jinsi gani tunaweza kuendelea kupanga vizuri ili nchi yetu iende mbele zaidi.



Wabariki kila mmoja ili wote wawe na afya njema, waweze kuendelea kushiriki vizuri kwa mipango yako. Kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu. Amina.

### **Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (Sheikh Kisusu Mvambo)**

Tufungue mikono yetu, pia tufungue na nyoyo zetu tuweze kumwelekea Mungu

Ewe Mwenyezi Mungu Muumba mbingu na dunia na vilivyomo kati yake. Tumekusanyika katika ukumbi huu wa Jakaya Kikwete kwa ajili ya kukuelekea wewe Mwenyezi Mungu na kukuomba. Mwenyezi Mungu tuko katika Mkutano wa 20 wa Taasisi zetu za Kifedha nchini. Tumekusanyika hapa, tunakuomba taasisi hizi tunaziweka mikononi mwako, mbele yako. Uzilinde kwa jicho lako lisilolala. Mwenyezi Mungu, tunakuomba nchi yetu ipate ufanisi, kwani bila uchumi mwema, hakutakuwa na ufanisi wa raia mmoja mmoja wala wa dola yenyewe. Tunakuomba taasisi zetu ziimarike na wasimamizi wa taasisi hizo uwape moyo wa uadilifu na ufanisi wa kutenda kazi.

Mwenyezi Mungu, tunafahamu kwamba ulimwengu umepata tikisiko la maradhi ya *Covid-19*. Maradhi ambayo yametikisa ulimwengu; yametikisa chumi za ulimwengu; na hata sisi Tanzania tumetikisika katika uchumi wetu. Mwenyezi Mungu leo tunakuomba, uchumi wetu uimarike na viongozi wetu wote, tunakuomba Mwenyezi Mungu uwape amani na salama, haswa, mbele yetu Rais wetu Mhe. Samia Suluhu Hassan. Mpe salama, mpe afya, mpe uwezo wa kuongoza nchi yetu ipate ufanisi na mafanikio ya umma kwa ujumla.

Mwenyezi Mungu tunakuomba haya kupitia heshima ya Mtume Mohammad S.A.W.

### **1.2 Salamu za Mkoa Kutoka kwa Mh. Anthony Mtaka, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma**

Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,  
Viongozi wote wa meza kuu,

Mhe. Rais naomba nifanye utambulisho mfupi wa viongozi wa mkoa ambao wamejumuika na wewe katika shughuli hii. Nao ni;

- Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma, Dkt. Fatma Mganga,
- Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Dodoma,
- Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Dodoma, Ndugu Godwin Mkanwa,
- Mkuu wa Wilaya ya Dodoma ambaye ni mwenyeji wetu, Kaka yangu Jabir Shekimweri,
- Machifu wetu, Chifu Mazengo na wenzake,
- Viongozi wetu wa Dini wa Mkoa wa Dodoma.

Mhe. Rais, shughuli hii ni ya kwako, kwa heshima na taadhima naomba ratiba iweze kuendelea.

### 1.3 Salamu Kutoka kwa Bw. Abdulmajid Nsekela, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Mabenki Tanzania

Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba, Waziri wa Fedha na Mipango

Mhe. Prof. Luoga, Gavana wa Benki Kuu

Viongozi wote walio meza kuu

Viongozi wote waliojumuika katika mkutano huu

Niseme tu itifaki imezingatiwa.

Kwanza kabisa nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutupa afya njema ya kufika siku ya leo ambapo tumekuja kwenye mkutano wetu mkuu ambao umeandaliwa na Benki Kuu.

Mhe. Rais, kipekee kabisa nichukue fursa hii kukushukuru sana wewe binafsi kwa kukubali mwaliko wa kuja kufungua mkutano huu pamoja na majukumu mengi uliyonayo ya kitaifa.

Mhe. Rais, tunafahamu kabisa, sekta ya fedha ni muhimu sana na ili ikue lazima sekta binafsi nayo iendelee kukua. Nichukue fursa hii, Mhe. Rais, kukushukuru sana kwa jitihada kubwa ambazo umezifanya za kuhakikisha sekta ya fedha inakua kwa kasi na kwa kufanya kazi kubwa ya kuweka sera nzuri zitakazofanya sekta binafsi ikue vilevile.

Mhe. Rais, tunafahamu mahusiano ya nchi mbalimbali ni muhimu. Nichukue fursa hii pia kukupongeza sana kwa kukuza diplomasia ya uchumi kwa nchi na nchi na kwa kujenga mahusiano makubwa kati ya Tanzania na mabara mengine duniani.

Mhe. Rais, mradi mkubwa ambao umeufanya hivi karibuni ni *Brand Tanzania*, na tuna imani utakapokamilika utakuwa ni kichocheo kikubwa cha kuleta wawekezaji wengi nchini na kufanya sekta ya benki kukua kwa sababu watakuwa wadau wakubwa sana.

Mhe. Rais, hivi karibuni umehudhuria *Conference of the Parties to the UN Framework Convention on Climate Change (COP26)*, kwa maana ya *Global Conservation Standard (GCS)* kuhusu masuala ya mazingira. Sisi tuliopo kwenye sekta ya fedha tumejipanga kuangalia fursa zinazotokana na mahusiano hayo ili tuweze kuzitumia kuleta maendeleo nchini Tanzania.

Mhe. Rais, nichukue fursa hii kipekee kuishukuru sana Benki Kuu. Tanzania imepita mazingira magumu kama nchi nyingine katika kipindi cha COVID-19; hata hivyo Benki Kuu ilisimama imara kwa kushirikiana na Jumuiya ya Mabenki kuangalia njia mbalimbali zitakazofanya sekta ya fedha iendelee

kuwa imara. Kwa kufanya hivyo, mabanki yote yameendelea kuwa imara, na yamefanya vizuri kwa mapato ya mwaka 2020, na hadi sasa yameendelea kufanya vizuri.

Mhe. Rais, kati ya mambo ambayo umesisitiza ni kuhakikisha taasisi za fedha zinawafikia Watanzania wengi; zinakuza utoaji mikopo kwa sekta binafsi na kwa riba nafuu. Niipongeze Benki Kuu, kwa kuchukua hatua mbalimbali zikiwemo za kisera ambazo zitaleta chachu ya mabanki kupunguza riba za mikopo wanayotoa. Hadi sasa, mabanki yamekuwa yakifanya *simulation* - kuja na taarifa rasmi ya kupunguza riba sehemu mbalimbali katika mikopo watakayotoa. Na hivi karibuni, utaanza kuona benki nyingi zikipunguza riba hizo.

Mhe. Rais, pamoja na hayo, tunafahamu kabisa nchi yetu ya Tanzania imepiga hatua katika kufikisha huduma za fedha kwa Watanzania wengi. Mafanikio hayo yamewezeshwa kwa kiasi kikubwa na matumizi ya teknolojia, ikiwemo kukuza mitandao ya uwakala wa mabanki. Aidha, benki zimejipanga kuhakikisha wakulima wengi wanafaidika au wanawezeshwa kimitaji ili kukuza uzalishaji na kipato chao.

Mhe. Rais, pamoja na jitihada zote hizi, na sera nzuri ambazo zimeendelea kutekelezwa, bado watanzania wachache wanaokopeshwa hawarejeshi mikopo inavyotakiwa. Hii inaleta changamoto kwa mabanki kukuza mikopo kwa wakopaji wengine. Kwa hesabu za hivi karibuni, ziko kesi zinazohusiana na mikopo yenye thamani ya Shilingi trilioni 1.2, katika hatua mbalimbali za kimahakama. Pamoja na changamoto hii tunakuahidi kwamba tutaendelea kuchangia juhudi za Serikali yako katika kusukuma gurudumu la maendeleo kwa kuwawezesha wananchi wengi kupata mitaji ambayo ni chachu ya ukuaji wa shughuli za kiuchumi.

Mhe. Rais, kwa mara nyingine, nichukue fursa hii kukushukuru sana wewe binafsi kwa kujumuika nasi leo kuja kufungua mkutano wetu na nimshukuru sana Mhe. Gavana kwa maandalizi yote aliyoyafanya katika mkutano huu.

Asante sana Mhe. Rais kwa kunisikiliza.

#### **1.4 Maneno ya Utangulizi Kutoka kwa Prof. Florens D.A.M. Luoga, Gavana Benki Kuu ya Tanzania**

Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), Waziri wa Fedha na Mipango

Mhe. Anthony John Mtaka, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma

Waheshimiwa Mawaziri mliopo

Waheshimiwa Makatibu Wakuu mliopo

Wakurugenzi wa Bodi ya Benki Kuu ya Tanzania

Manaibu Gavana wa Benki Kuu Bwana, Julian Raphael Banzi, Dkt. Yamungu Kayandabila na Dkt. Bernard Kibesse

Wakuu wa Taasisi za Fedha

Watoa Mada katika Mkutano huu

Wageni Waalikwa

Mabibi na Mabwana

### **Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

#### **Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**



**Prof. Florens Luoga akizungumza wakati wa mkutano**

Ninayo furaha na heshima kubwa kukukaribisha katika Mkutano huu wa 20 wa Taasisi za Fedha nchini. Aidha, napenda kutoa shukrani zangu za kipekee kwako, kwa kukubali kufungua Mkutano huu, licha ya ratiba yako yenye shughuli nyingi. Vilevile, napenda kumshukuru Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri wa Fedha na Mipango wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kujumuika nasi katika mkutano huu. Shukrani za dhati pia ziende kwa uongozi wa Jiji letu na Makao Makuu, Dodoma, kwa

kutukaribisha, kutuhakikishia usalama wetu na kutenga muda wao kushiriki nasi katika tukio hili. Aidha, tunawashukuru watoa mada na wageni waalikwa kwa kukubali mwaliko wetu.

#### **Mhe. Rais, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana,**

Mkutano wa mwaka huu unafanyika wakati nchi yetu inatarajia kuadhimisha miaka 60 tangu tupate uhuru, tarehe 9 Desemba 1961. Hakika, nchi yetu imepata mafanikio makubwa katika nyanja mbalimbali. Kwa upande wa uchumi, nchi yetu imeweza kufikia kuwa nchi ya kipato cha kati, mwezi Julai 2020, ikiwa na kipato cha wastani wa dola za Marekani 1,080. Mafanikio haya yamewezeshwa, pamoja na mambo mengine, na ukuaji endelevu wa uchumi, utulivu wa bei za bidhaa na huduma, na utulivu katika mwenendo wa thamani ya shilingi dhidi ya fedha za kigeni. Kutokana na mipango madhubuti ya kiuchumi, kama ilivyo ainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Awamu

ya Tatu, ni matarajio yetu kuwa Tanzania itaendelea kupiga hatua kubwa za maendeleo ya kiuchumi baada ya janga la UVIKO-19.

Aidha, Mkutano huu unafanyika katika mazingira ambayo dunia bado inakabiliwa na janga la UVIKO-19, hivyo, tumejipanga kuufanya Mkutano wetu kwa njia ya ana kwa ana (kama tulivyo hapa ukumbini) na kwa njia ya mtandao. Hivyo basi, baadhi ya watoa mada na washiriki wengine watahudhuria Mkutano huu kwa njia zote mbili. Niwahakikishie wote kuwa, tumefanya kila jitihada kuhakikisha mkutano huu unafanikiwa.

Vilevile, Mkutano wa mwaka huu ni wa muhimu kwa sababu wadau wa sekta ya fedha wanaadhimisha miongo minne ya Mkutano wa Taasisi za Fedha, tangu kuanzishwa kwake, Mei 1980. Mkutano wa Taasisi za Fedha umekuwa jukwaa la wakuu wa taasisi za fedha, wasomi, na watendaji kukutana na kujadili masuala yanayohusu maendeleo ya sekta ya benki, sekta ya fedha na uchumi kwa ujumla. Katika kipindi cha miongo minne iliyopita, tumeweza kufanya mikutano 19 kujadili masuala mbalimbali, ambayo kwa kiasi kikubwa yaliakisi mahitaji ya wakati huo.

#### **Mhe. Rais, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana,**

Kama nilivyoeleza hapo awali, mkutano wa mwaka huu unafanyika katika mazingira ambayo nchi yetu imepata changamoto ya janga la UVIKO-19, ambalo limesababisha athari kubwa za kiuchumi na kijamii. Tunafurahi kuona kuwa athari za janga hili zinapungua na hivyo kutoa mwanga wa matumaini wa kuimarika kwa uchumi. Hali hii inachangiwa na ongezeko la utoaji wa chanjo ya UVIKO-19 na jitihada nyingine za kuimarisha uchumi zinazochukuliwa na Serikali, sekta binafsi na wadau wa maendeleo. Kwa kuzingatia umuhimu wa kukuza uchumi na maendeleo ya teknolojia, tuliona ni vema kuwa na mjadala wa kina kuhusu hatua zinazofaa kuimarisha uchumi na namna ambavyo nchi yetu inaweza kunufaika na maendeleo ya teknolojia. Kwa mantiki hii, tumeandaa mkutano huu wenye dhima: **"Kuimarika kwa Uchumi wa Tanzania kutoka katika Janga la UVIKO-19 na hali ya Baadaye"**. Katika dhima hii, washiriki watajadili masuala mbalimbali yanayogusa maeneo makuu manne, ambayo ni:

- i. Ukuaji wa uchumi endelevu wakati na baada ya janga la UVIKO -19: Vipaumbele na sera mbadala;
- ii. Kuchochea kasi ya maendeleo ya kidijitali katika kuimarisha ukuaji endelevu wa uchumi;
- iii. Sarafu za kidijitali: Uzoefu, vihatarishi na usimamizi; na
- iv. Kuongeza mikopo kwa sekta binafsi baada ya janga la UVIKO-19: Wajibu wa serikali, taasisi za fedha na sekta binafsi.

Mada hizi nne zinahusu hitaji la kufikiria upya jinsi ya kuwezesha uimarishaji wa haraka wa uchumi na kuhakikisha ukuaji endelevu wakati na baada ya UVIKO-19. Katika muktadha huo, Mkutano huu umejumuisha washiriki kutoka ndani na nje ya nchi wenye ujuzi na uzoefu wa hali ya juu katika ajenda ya maendeleo. Tumaamini kuwa, mchanganyiko huu wa uwakilishi utatoa ushauri sahihi wa kisera ambao utachangia kuisukuma sekta yetu ya fedha na uchumi kwa ujumla katika njia zilizo endelevu.

**Mhe. Rais, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana,**

Kama tunavyofahamu sote, Tanzania haikuepuka athari za kiuchumi zilizosababishwa na janga hili la UVIKO-19, licha ya kuchukua uamuzi wa kutokuzuia au kufunga shughuli za uchumi (*lockdown*). Kasi ya ukuaji wa uchumi ilipungua hadi kufikia asilimia 4.8 mwaka 2020, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 6.8 miaka mitano iliyopita. Sekta ya utalii, ambayo imekuwa moja ya vyanzo vikubwa vya mapato ya fedha za kigeni, iliathiriwa zaidi na janga hili, kwani mapato yake yalipungua kwa zaidi ya nusu na kufikia dola za Marekani milioni 714.5 mwaka 2020. Hali hii ilitokana na kupungua kwa idadi ya watalii kwa asilimia 60 na kufikia 620,867. Aidha, ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi ulipungua hadi asilimia 4.3 mwaka 2020/21 ikilinganishwa na asilimia 8.1 mwaka 2019/20, kutokana na kushuka kwa mahitaji ya mikopo na kuongezeka kwa vihatarishi vya mikopo kwa wakopaji (*credit risks*).

**Mhe. Rais,**

Nina furaha kuripoti kwamba nchi yetu ilikuwa miongoni mwa nchi chache zilizoepuka mpororo wa uchumi mwaka 2020, na uchumi wetu unatarajiwa kukua kwa asilimia 5 mwaka 2021. Mfumuko wa bei umebakia kuwa ndani ya lengo la asilimia 3-5 na kuendana na lengo la Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) lililozidi asilimia 8, na asilimia 3-7 kwa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC). Mfumuko wa bei unatarajiwa kuwa ndani ya lengo la asilimia 3-5 kwa mwaka 2021/22, licha ya ongezeko la bei za mafuta katika soko la dunia. Thamani ya Shilingi dhidi ya dola ya Marekani imeendelea kuwa thabiti wakati wote wa janga hili, ikipungua thamani kwa kasi ndogo ya chini ya asilimia moja kwa mwaka. Akiba ya fedha za kigeni imeendelea kuwa ya kutosha, na hivyo kuifanya nchi iwe na uwezo wa kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje kwa zaidi ya miezi mitano, ikilinganishwa na lengo la miezi minne. Hivi sasa akiba ya fedha za kigeni inaweza kutosheleza uagizaji wa bidhaa kutoka nje kwa zaidi ya miezi sita.

Sekta ya benki inaendelea kuwa thabiti, yenye faida, na yenye mtaji wa kutosha. Kutokana na muda, napenda kutaja viashiria vichache, kama ifuatavyo;

- Benki zimekuwa na mitaji ya kutosha, ambapo mtaji mkuu (*core capital*) na mtaji wa jumla (*total capital*) ulikuwa wastani wa zaidi ya asilimia 17.1 na asilimia 17.9 mwezi Juni 2021, ikilinganishwa na lengo la asilimia 10 na asilimia 12, mtawalia.

- Uwiano wa ukwasi (*liquid assets*) na amana za muda mfupi (*demand liabilities*) ulikuwa asilimia 33.3 mwaka 2020/21, ukilinganishwa na kiwango kinachohitajika cha asilimia 20. Hivyo, mabanki yalikuwa na ukwasi wa kutosha wa kutoa mikopo kwa sekta banafsi.
- Mikopo chechefu (*non-performing loans*) ilipungua hadi asilimia 9.3 mwezi Juni 2021 kutoka asilimia 10.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2020, ingawa bado ni juu ya kiwango kinachokubalika cha asilimia 5. Katika kupunguza mikopo chechefu, Benki Kuu ya Tanzania imeelekeza benki na taasisi nyingine za fedha nchini kuchukua hatua za haraka za kupunguza mikopo chechefu na riba. Aidha, Benki Kuu imeelekeza taasisi hizo kuboresha taratibu za utoaji wa mikopo, matumizi ya mfumo wa kumbukumbu za mikopo, na kuimarisha juhudi za kurejesha mikopo.

**Mhe. Rais,**

Matarajio yetu ni kuwa, uchumi wa Tanzania utakua kwa kasi, na kufikia zaidi ya asilimia 8 katika miaka mitano ijayo. Makadirio haya yanatokana na kuongezeka kwa matumizi ya rasilimali na ongezeko la tija katika shughuli za uzalishaji. Ni kutokana na hali hii tumeandaa mada muhimu kuhusu **"Ukuaji wa Uchumi Endelevu Wakati na Baada ya Janga la UVIKO-19: Vipaumbele na Sera Mbadala"**. Hivyo basi, mkutano huu unatarajiwa kujadili mada hii na kubainisha msukumo wa kisera unaohitajika ili kufikia ukuaji unaotarajiwa. Ni matumaini yetu kuwa watoa mada na wageni waalikwa wana uzoefu na utaalamu wa kutosha wa kuchangia katika mada hii.

**Mhe. Rais,**

Ili kusaidia kuimarika kwa uchumi na kuhakikisha kuwa ukuaji unakuwa endelevu, Benki Kuu ya Tanzania imetekeleza hatua kadhaa za kisera zinazolenga kupunguza riba za mikopo, kuongeza ukwasi katika mabanki, kuongeza mikopo kwa sekta ya kilimo, na kuhamasisha matumizi ya mifumo ya malipo ya kidijitali. Hatua hizo ni pamoja na:

- a. Kupunguza kiwango cha kisheria cha sehemu ya amana kinachotakiwa kuwekwa Benki Kuu na benki za biashara (*Statutory Minimum Reserve*) kutoka asilimia 7 hadi asilimia 6 kuanzia tarehe 8 mwezi Juni 2020, na hivi karibuni kutoa unafuu kwa benki zitakazotoa mikopo kwenye sekta ya kilimo kwa riba isiyozidi asilimia 10.
- b. Kuongeza ukomo wa miamala ya kila siku kwa mteja wa huduma ya fedha kwa njia ya kidijitali kutoka shilingi milioni 3 hadi shilingi milioni 5 na kuongeza kiwango cha salio kwa mteja kutoka shilingi milioni 5 hadi shilingi milioni 10.
- c. Kutoa unafuu wa mahitaji ya kiusimamizi katika kufanya marekebisho ya marejesho ya mikopo (*loan restructuring*) kwa wateja wa mabanki na taasisi za fedha walioathirika na janga la UVIKO-19, ili kuwawezesha wateja hao kulipa mikopo bila kuathiri biashara au miradi yao.

- d. Kuondoa sharti la uzoefu wa kufanya biashara kwa angalau miezi 18 kwa waombaji wa biashara ya wakala wa mabenki. Badala yake, waombaji wa uwakala wa mabenki watatakiwa kuwa na kitambulisho cha taifa au namba ya kitambulisho cha taifa.
- e. Kuanzisha mfuko maalum wenye thamani ya shilingi trilioni moja ambao utatumika kukopesha mabenki na taasisi za fedha kwa riba ya asilimia 3, ili taasisi hizo ziweze kukopesha sekta ya kilimo kwa riba isiyozidi asilimia 10 kwa mwaka.

Ni matumaini yetu kwamba mabenki na taasisi nyingine za fedha zitaendelea kuunga mkono juhudi zetu kwa kupunguza riba za mikopo na kuboresha huduma za kifedha. Hivyo basi, ili kuchochea ushirikiano zaidi, tulichagua kupitia mkutano huu tujadili mada kuhusu **“Kuongeza Mikopo kwa Sekta Binafsi Baada ya Janga la UVIKO-19: Wajibu wa Serikali, Taasisi za Fedha na Sekta Binafsi”**.

#### **Mhe. Rais,**

Maendeleo ya teknolojia ya kidijitali yanazidi kushika kasi duniani kote huku yakiathiri jinsi tunavyofanya biashara katika sekta mbalimbali za uchumi. Aidha, maendeleo hayo yanabadilisha namna ambayo watu wanafikia na kutumia huduma za fedha, huku bidhaa na mifumo mipya ya fedha za kidijitali ikiibuka kwa kasi. Katika kusaidia maendeleo ya mifumo ya kidijitali, Benki Kuu ya Tanzania imekuwa ikiweka mazingira wezeshi ya usimamizi katika sekta ya fedha. Mafanikio yaliyopatikana kutokana na kuwepo kwa mfumo wa usimamizi ni kuongezeka kwa ubunifu katika huduma za fedha kupitia simu za kiganjani na huduma za kibenki. Hali hii imechangia kuongezeka kwa huduma za fedha kwa njia ya simu, hivyo kurahisisha shughuli za kiuchumi na kuongezeka huduma jumuishi za fedha. Mojawapo wa mafanikio hayo ni kuongezeka kwa namba za akaunti hai za wateja katika mitandao ya simu za kiganjani kufikia milioni 31.5 mwezi Juni 2021, ikiwa ni ongezeko la asilimia 42 kutoka Juni 2020. Aidha, kulikuwa na ongezeko la asilimia 22.9 la idadi ya mawakala wanaotoa huduma za fedha kwa kutumia simu za kiganjani hadi 767,117. Vilevile, tumeshuhudia ongezeko la matumizi ya teknolojia katika shughuli za kibenki, ikiwemo huduma za kifedha na mifumo mbalimbali ya malipo.

Katika jitihada za kuongeza ufanisi na kupunguza gharama katika huduma za malipo ya kimtandao, Benki Kuu kwa kushirikiana na wadau imetengeneza mfumo wa kitaifa wa malipo ya reja reja (*Tanzania Instant Payment System-TIPS*) ili kupunguza gharama kwa watumiaji. Mfumo huo ulikamilika Julai 2021, na hivi sasa upo kwenye hatua za majaribio. Aidha, Benki Kuu inashirikiana na *Financial Sector Deepening Trust* (FSDT) kutengeneza kanzidata ya watoa huduma za fedha kwa ajili ya kujua maeneo yaliyofikiwa na huduma za fedha na kubaini kimtandao maeneo ambayo bado hayajafikiwa na huduma za fedha. Hivyo basi, ili kuhakikisha nchi yetu inaendelea kunufaika na maendeleo ya teknolojia, tuliamua kuwa na mada kuhusu: **“Kuchochea Kasi ya Maendeleo ya Kidijitali kwa Ajili ya Ufufuaji na Ukuaji Endelevu wa Uchumi”**.



**Mhe. Rais,**

Maendeleo ya teknolojia ya kidijitali katika sekta ya fedha pia yamepelekea kuibuka kwa sarafu ya kidijitali ya benki kuu (*Central bank digital currency—CBDC*) na sarafu-fiche (*crypto currencies*) zinazotolewa na watu au kampuni binafsi. Benki kuu kadhaa duniani zimeanza kushiriki katika maeneo haya kwa njia mbalimbali. Kwa CBDC, benki kuu ziko katika hatua mbalimbali za kutengeneza sarafu zao za kidijitali. Mfano, Benki Kuu ya Nigeria imezindua *eNaira* hivi karibuni, hivyo kuwa Benki Kuu ya kwanza barani Afrika kuzindua CBDC. Katika kuhakikisha nchi yetu haibaki nyuma, Benki Kuu ya Tanzania imeshaanza maandalizi ya uwezekano wa kuwa na CBDC. Maandalizi hayo yanahusisha kujenga uwezo kwa wataalamu, kuongeza ufahamu kwa wadau na kufanya tafiti. Kuhusu sarafu za mtandaoni zinazotolewa na watu au kampuni binafsi, Benki Kuu ya Tanzania imetoa tahadhari kwa umma kuhusu athari zinazoweza kupatikana kwa kujihusisha na sarafu hizo. Kwa kuzingatia umuhimu wa maendeleo katika anga ya kidijitali, tuliona ni muhimu kuwa na mada katika mkutano huu kuhusu: **“Sarafu za Kidijitali: Uzoefu, Vihatarishi na Usimamizi”**.

**Mhe. Rais,**

Kwa miaka mingi, benki kuu zimekuwa zikihifadhi dhahabu, kama sehemu ya akiba ya fedha za kigeni. Kwa mujibu wa miongozo ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), dhahabu inayostahili kuhifadhiwa kama akiba ya fedha za kigeni lazima iwe na kiwango cha ubora kisichopungua asilimia 99.5. Dhahabu yenye ubora huo inajulikana kama *monetary gold*.

Katika azma ya kuboresha akiba ya fedha za kigeni nchini, na kwa kuzingatia kuwa bei ya dhahabu katika soko la dunia imekuwa ikiongezeka kwa miaka ya hivi karibuni, Benki Kuu ya Tanzania inaendelea na maandalizi ya kununua dhahabu yenye ubora unaotakiwa kutoka viwanda vya kusafisha dhahabu vilivyopo hapa nchini. Kiasi cha dhahabu kitakachonunuliwa kitazingatia lengo la kuimarisha akiba ya fedha za kigeni na lengo la sera ya fedha la kudhibiti mfumuko wa bei. Kwa hiyo, mafanikio ya Benki Kuu katika kununua dhahabu yanategemea kasi ya viwanda vyetu kuanza kuzalisha dhahabu yenye ubora unaohitajika.

Nichukue fursa hii kukupongeza, **Mhe. Rais**, kwa juhudi zako zilizofanikisha kupatikana kwa mkopo wa masharti nafuu kutoka IMF kwa ajili ya kushughulikia changamoto za UVIKO-19. Kupitia juhudi zako, Serikali iliweza kupata dola za Marekani milioni 567.25 kutoka IMF mwezi Septemba 2021. Fedha hizo zimesaidia kuimarisha akiba ya fedha za kigeni. Hii inaonesha dhamira yako ya dhati katika kuhakikisha uchumi wetu unakua kwa kasi zaidi.

Ninapenda kukuhakikishia, **Mhe. Rais**, Benki Kuu ya Tanzania itaendelea kuhakikisha mfumuko wa bei unakuwa wa kiwango cha chini, thamani ya Shilingi dhidi ya fedha za kigeni inaendelea kuwa imara, na mabanki yetu yanakuwa na ukwasi wa kutosha ili kuongeza mikopo kwa sekta binafsi na kuchangia ukuaji wa uchumi.

**Mhe. Rais,**

Naomba nimalizie hotuba yangu kwa kurudia kutoa shukrani zangu kwako kwa kutenga muda wako kuja kutufungulia Mkutano huu. Ni matumaini yetu kuwa Mkutano huu, kama ilivyokuwa mikutano iliyotangulia, utakuwa na mafanikio makubwa, kwa kuwa utatoa fursa ya kipekee kwa taasisi za fedha na wadau wengine kutoa uzoefu wao kuhusu mada zitakazojadiliwa katika **Mkutano huu wa 20 wa Taasisi za Fedha**.

**Mhe. Rais**, kwa rufusa yako, sasa naomba nimkaribishe Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), Waziri wa Fedha na Mipango, aweze kutoa hotuba yake na kukukaribisha kuzungumza.

**Mhe. Rais, Nashukuru Sana! Asante!**

## 1.5 Salamu za Ukaribisho kutoka kwa Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba, Waziri wa Fedha na Mipango

Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Mhe. Profesa Florens Luoga, Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania

Mhe. Anthony John Mtaka, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma

Wenyeviti wetu wa Kamati, Kamati ya Bajeti na Kamati ya Uchumi

Waheshimiwa Mawaziri wenzangu na Manaibu mliohudhuria tukio la leo

Waheshimiwa Wabunge

Makatibu wakuu na Manaibu Katibu Wakuu mliopo.

Wakurugenzi wa Bodi ya Benki Kuu

Manaibu Gavana

Wakuu wa Taasisi za Fedha

Ndugu yetu CAG

Viongozi wengine wa Serikali mliopo

Niliona na rangi ya kijani mahali, Viongozi wa CCM

Viongozi wetu wa Kidini

Viongozi wetu wa vyombo vya dola

Watoa Mada wa Mkutano huu

Wageni Waalikwa

Mabibi na Mabwana.

Nawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

### **Mhe. Rais,**

Napenda kukuaribisha katika Mkutano huu wa 20 wa Taasisi za Fedha nchini. Vilevile, napenda kukushukuru kwa dhati kwa kutenga muda wako kushiriki Mkutano huu muhimu na kwa kukubali kuwa Mgeni Rasmi licha ya majukumu yako mengi muhimu uliyonayo. Kama alivyosema Gavana wa Benki Kuu, Mkutano huu unafanyika kwa mara ya kwanza hapa Dodoma, Makao Makuu ya Nchi, tangu mwaka 1980 wakati jambo hili linaasisiwa. Makao Makuu ya Nchi, Dodoma, yana sifa za kipekee kwani ndiyo katikati ya nchi yetu, na hivyo kuwa na nafasi kubwa ya kufikiwa kwa urahisi na maeneo mengine na hata upande wa wawekezaji. Kwa sababu hii, naipongeza Benki Kuu na taasisi za fedha nchini kwa kuandaa Mkutano huu na kuandika historia katika jiji letu la Dodoma.

**Mhe. Rais,**

Wizara ya Fedha na Mipango inatambua kwamba juhudi zaidi zinahitajika kurudisha uchumi wetu katika ukuaji tuliokuwa nao kabla ya janga la UVIKO-19 na kuupeleka kwenye hadhi ya uchumi wa kati wa juu kwa haraka zaidi. Naamini Mkutano huu utatoa fursa ya kushirikishana mawazo na uzoefu juu ya mbinu zinazoweza kutumika kufikia lengo hili pana na muhimu sana kwa nchi yetu.

Nitoe tu changamoto kwa wenzetu mabenki. Mabenki ya biashara yaongeze ubunifu na kuleta mapendekezo ya kisera wizarani ili tuweze kuongeza utoaji mikopo kwa sekta binafsi kwenye maeneo makubwa ya kiuchumi kama ya kilimo, mifugo, uvuvi pamoja na sekta nyingine ambazo ni kichocheo cha kukua kwa haraka kwa uchumi.

Pia, waangalie kuweka ubunifu kwa ajili ya kundi kubwa la vijana wanaoshindwa kujiajiri kwa kukosa mitaji ya kuanzisha biashara. Hili ni kundi kubwa sana na tunakaribisha mawazo hayo ya kisera hapa wizarani, ili tuweze kupata suluhisho la changamoto ya mitaji kwa vijana wanaoanzisha biashara kwa sababu ya kukosa mitaji na huku wakiwa na changamoto kubwa ya masuala ya ajira. Mabenki na taasisi za fedha wafanye haraka tukae, na ikiwezekana tunavyokwenda kwenye mwaka wa fedha mwingine tuwe na jambo ambalo tunaweza tukalisema la kisera kuwasaidia vijana kupata mitaji kwa njia ambayo itawawezesha wengi wavutike kwenda sekta binafsi, na pengine kujiajiri au kuanza kutengeneza ajira za wengine. Vijana wengi wakinufaika na fursa hizi itachangia kukua kwa uchumi kwa kasi kubwa zaidi.

**Mhe. Rais,** kabla sijakukaribisha, naomba pia uniruhusu nikupongeze kwa kuiongoza nchi yetu katika mwelekeo sahihi kisiasa, kijamii na kiuchumi. Hakika, umeonesha umahiri mkubwa sana kuhakikisha uchumi wetu unavuka salama katika kipindi hiki cha changamoto za janga la UVIKO-19, na pia, mwelekeo sahihi wa kule tunakoelekea.

**Mhe. Rais,**

Wengine wanaweza wasione muunganiko huo wa kiuchumi wa kazi hizi unazofanya. Jambo la kwanza, fedha unazopeleka kwa ajili ya miradi ya maendeleo, ukiwauliza halmashauri karibu zote



***Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, Dkt. Mwigulu Nchemba***

wanasema fedha walizopokea katika miezi sita tu iliyopita, hazijawahi kutokea! Hivi sasa, wilaya zote haziazimani mafundi; kila wilaya na kata ziko bize na shughuli katika maeneo yao na hii inaongeza mzunguko wa fedha na hata fedha kwa mtu mmoja mmoja kwa sababu kazi hizi zinafanywa na watu wetu.

Mhe. Rais, jambo lingine ulilolifanya, ambalo litafungua fursa kubwa zaidi za kiuchumi kwa watu wetu, ni kulipa madeni kwa watoa huduma wadogo wadogo. Tayari zaidi ya Shilingi bilioni 22 zimekwenda kulipa wazabuni na watoa huduma wadogo wadogo, hususan kwa shule za msingi na sekondari. Aidha, madeni mengine yaliyolipwa ni ya watumishi zaidi ya Shilingi bilioni 24, wazabuni waliotoa huduma ya chakula kwa vyombo vyetu vya ulinzi na usalama (Shilingi bilioni 40); wakandarasi (Shilingi bilioni 69); na waliotoa huduma kwa mamlaka za maji, umeme, simu (Shilingi bilioni 13).

Mhe. Rais, hawa ni watu ambao umegusa maisha yao kwani wengine walishakata tamaa kulipwa fedha zao. Na ulipoingia madarakani ulituuliza Wizara ya Fedha maswali haya: Hata hamuoni huruma? Hawa ni watu wadogo kabisa walishatoa huduma kwa Serikali halafu hamuwalipi, kwa nini? Mhe. Rais, fedha hizi zimeshalipwa na kwa ushuhuda wengine wanatutumia ujumbe wakisema tukuletee salamu na pongezi kwa jambo hili. Fedha hizi zimekwenda moja kwa moja kwenye mzunguko na hivyo kuchochea ukuaji wa uchumi na kipato kwa wananchi.

**Mhe. Rais**, ulielekeza tunapokusanya kodi tusifunge akaunti za watu. Jambo hili limetekelezwa na kuleta furaha na faraja kwa wafanyabiashara. Vilevile, kwa kuwa tumeelezwa kwamba riba zitaendelea kupungua, rai yangu kwa wafanyabiashara ni waendeleo kutumia mablenki kwani ndio utaratibu wa kisasa wa kuendesha uchumi. Aidha, natoa wito kwa wakopaji kulipa madeni wanayodaiwa na mablenki na taasisi za fedha kwani kutokufanya hivyo inapunguza fursa ya wengine kukopa.

**Mhe. Rais,**

Kabla sijamaliza, nitumie fursa hii pia kuwashukuru na kuwapongeza Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) kwa fedha walizotupatia za masharti nafuu kabisa ambazo ulielekeza zitatue changamoto za huduma za jamii zinazotokana na janga la UVIKO-19. Fedha hizo ni fedha ambazo hazina riba. Ni mkopo ambao una masharti nafuu.

Katika kumalizia, Mhe. Rais, *audience* yetu ina mchanganyiko. As you may see, we have a mixed audience, unfortunately all of them will prefer to hear and understand directly as you address, some in favour of Kiswahili and others in favour of English. Madam President, may it please you to use both of the languages as it may be convenient to you. Please, our apologies for that. Tunakuomba sana ikupendeze tu utumie lugha zote kadri utakavyoona inafaa, ili kila mmoja akupate moja kwa moja wakati ukihutubia.

Baada ya kusema hayo nichukue heshima hii kukukaribisha ili uweze kuhutubia.

Karibu sana Mhe. Rais.

## 1.6 Hotuba ya Ufunguzi ya Mgeni Rasmi, Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba, Waziri wa Fedha na Mipango

Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro, Waziri wa Maliasili na Utalii

Prof. Florens Luoga, Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania

Manaibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania

Mhe. Anthony Mtaka, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma

Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa wa Dodoma

Waheshimiwa Wabunge mliopo

Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama mliopo

Bodi ya Wakurugenzi ya Benki Kuu

Wakuu na Wawakilishi wa Taasisi za Fedha

Watoa Mada

Mwenyekiti wa Umoja wa Mabenki

Wakuu wa Mabenki Mliopo

Bw. Charles Kichere, Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

Viongozi wa Dini Mliopo

Machifu wenzangu mliopo

Wageni waalikwa

Mabibi na Mabwana



**Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan akihutubia Mkutano**

### **Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!**

Nilitayarisha hotuba yangu kwa Kiingereza kwa sababu niliambiwa mkutano huu una washiriki kutoka nje ya nchi wakishiriki nasi hapa na kwa njia ya mtandao. Nitajitahidi kutoa hotuba yangu kwa Kiswahili na Kingereza.

